

Watakatifu ni pamoja na wanaomtumikia Bwana

Na Mchg. Profesa Gwakisa E. Mwakagali

Kwa kufuata Kalenda ya Biblia ya KKKT, Siku ya Watakatifu inaadhimishwa Jumapili ya kwanza ya Novemba kila mwaka. Mwaka 2014 iliadhimishwa Novemba Pili.

Kanisa la Mwanzo

Swali linalojitokeza hapa ni: Hao Watakatifu ni akina nani? Na kwa nini wanakumbukwa? Dini nyingi zilizopo ulimwenguni zina watakatifu wao wanaokumbukwa na kuheshimiwa na hata kuabudiwa. Wabuda na Wahindu wana watakatifu wao. Katika Kanisa la kwanza (The Early Church) lilifundisha: “Wakristo waaminifu katika ulimwengu huu walikuwa sehemu ya ‘Ushirika wa Watakatifu’.

Katika imani ya Kanisa Katoliki, ‘Mtakatifu’ ni mtu yeyote aliyetangazwa rasmi na kanisa kwamba ni Mtakatifu na anaaminika kuwa yuko mbinguni hivyo anapaswa kuheshimiwa (venerate) na wakristo na kanisa kwa ujumla (siyo kuabudiwa). Watakatifu hao wanakumbukwa kwa kuigwa mfano wa maisha ya uaminifu na uchaji kwa Mungu. Ni imani ya Kanisa Katoliki kwamba watakatifu wanauwezo wa kuwaombea wakristo kwa Mungu na baadhi ya Watakatifu wanahesabiwa kuwa walenzi wa wakristo walio hai.

Kati ya watakatifu wanaotambulika na Kanisa Katoliki ni pamoja na Mariamu mama yake Yesu ambaye anaitwa ‘Mama Mtakatifu’ na ‘Mama wa Mungu’. Na Papa anaitwa Baba Makatifu kwa kuwa ni mrithi wa kiti cha Mtume Petro Mtakatifu na mwakilishi wa Kristo ulimwenguni.

Kwa Walutheri na makanisa yenye mfumo wa Kiinjili, watakatifu ni wanadamu wenye dhambi wanaostahili msamaha wa dhambi zao. Kufuata imani ya Kilutheri haijaandikwa popote katika Maandiko Matakatiifu (Biblia) kwamba tunapaswa kuwaomba ama kutafuta msaada wa kiroho kutoka watakatifu.

Wala haijaandikwa lolote kuhusu kuwaomba watuombea kwa Mungu, kufunga kwa ajili yao wala kuadhimisha sikukuu kwa ajili ya kila mmoja wao kama wafanyavyo wenzetu wakatoliki na makanisa mengine ya Ulaya, wala kutoa sadaka kwa ajili yao na wala kuanzisha huduma yoyote kwa ajili yao. Mambo hayo yangekuwa ni sawa na kuabudu sanamu (idolatry).

Maana ya watakatifu kwa Kanisa la Kilutheri ni wale wote wanaoshiriki kuitangaza Injili ya Kristo na kufundisha kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Katika jumuiya hiyo wako waliotangulia (walio kufa) na wako walio hai. Hiyo ndiyo maana ya maneno: ‘Ushirika wa Watakatifu’ katika Ukiri wa Imani ya Mitume. Pia Watakatifu ni wale wote wanaomwamini Bwana wetu Yesu Kristo, yaani ‘waaminio’ wote.

Katika Biblia tunasoma Anania anavyosema “Bwana nimesikia habari za mtu huyu ... alivyowatenda ‘Watakatifu’ wako Yerusalemu” (Mdo 9: 13, 32, 41; Mdo 26: 10).

Mtume Paulo aliwaita wakristo wa Usharika wa Rumi: “Wapendwao na Mungu, walioitwa kuwa ‘watakatifu’ maana imewapendeza watu wa Makedonia na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya ‘watakatifu’ huko Yerusalemu walio maskini” (Warumi 15: 25 - 26).

Paulo aliwaita wakristo wa Korintho: “...Wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe ‘waakatifu’ pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo” (1Kor 1: 2). Paulo anawataka wakristo kushtakiana mbele ya ‘watakatifu’ na siyo mbele ya wasio haki kwa maana watakatifu watauhukumu ulimwengu (1Kor 6: 1 - 2). Katika Ufunuo Yohana anaeleza kuwa maombi ya ‘watakatifu’ ni manukato (Ufunuo 5: 8).

Makanisa ya Kiprotestanti huadhimisha Sikukuu ya Watakatifu ili kuwakumbuka waliomwamini Bwana Yesu Kristo, wakaitangaza habari njema ya wokovu katika jina lake na kuishi maisha ya uaminifu na uchaji na kumpendeza Mungu. Kati yao wamo Mitume na wale Mashahidi wa maisha na kazi ya Yesu Kristo hapa duniani.

Wamo pia watumishi wa Mungu ngazi mbalimbali waliotenda kazi yake kwa uaminifu na walioishi maisha ya kumpendeza Mungu na kuwa mfano wa kuigwa katika ulimwengu. Katika hao wamo wazee, Wainjilisti, Wachungaji, Maaskofu na watumishi mbalimbali katika kanisa.

Wamo pia wakristo raia walioishi maisha ya uaminifu na uchaji wakawa mfano wa kuigwa katika jamaa zao, jamii na ulimwengu kwa jumla. Wengi wao wamelala mauti wakingoja siku ya kuja kwa Bwana wetu katika utukufu.

Pia tumo sisi tulio hai wakati huu tukiendelea kumtumikia Bwana kwa njia mbalimbali na kuishi kwa uaminifu na uchaji katika ulimwengu wa sasa hadi Kristo atakaporudi. Sikukuu ya Watakatifu pia itukumbushe juu ya uenyeji wetu wa mbinguni. Bwana akubariki!

(Profesa Mwakagali ni Mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira anapatikana sms: 0784 431 343 au 0715 932 806)